# JARIDA MAALUM

## OFISI YA WAZIRI MKUU
## KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU

**Toleo No. 1** **Novemba, 2020**





# SERIKALI YAJIZATITI KUKUZA SOKO LA AJIRA

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli ameeleza kuwa katika miaka mitano ijayo Serikali anayoiongoza imekusudia kuendeleza mafanikio ya kiuchumi yaliyopatikana ili kuhakikisha ukuaji wa uchumi unawanufaisha wananchi kwa kuinua vipato vyao, kupunguza umaskini na tatizo la ajira.

Ameeleza hayo wakati akifungua Bunge la 12 Jijini Dodoma. Mheshimiwa Rais, Dkt. Magufuli amesema Serikali imelenga kukuza uchumi kwa wastani wa angalau asilimia 8 kwa mwaka na pia kutengeneza ajira mpya zipatazo milioni 8.

Sambamba na hilo, Rais Magufuli alieleza kuwa Serikali itaongeza jitihada za kuwawezesha wananchi wetu kiuchumi kwa kuwapatia mikopo isiyo na riba ama yenye riba nafuu, ikiwemo mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na Halmashauri zetu; na pia kupitia Mifuko na Programu mbalimbali zilizoanzishwa na Serikali, ambayo kwa idadi zipo 18.

“Tutaimarisha usimamizi wa Mifuko hii na kuhakikisha Watanzania wanaifahamu, Nataka Mifuko hii ikiwasaidie wananchi wa kawaida, wakiwemo machinga, akina baba na mama lishe pamoja na wajasiriamali wengine wadogo.” ameeleza

Pamoja na hayo, tutaendelea kutekeleza Program mbalimbali za kukuza ujuzi na maarifa, ikiwemo maarifa ya ujasiriamali, ili kuwapa ujuzi na uzoefu wananchi wetu utakaowawezesha kujiajiri ama kuajirika ndani na nje ya nchi.



# WAZIRI MKUU MAJALIWA AHAIDI KUFANYA KAZI KWA BIDII

Kura za Wabunge 350 zilizopigwa (Novemba 12, 2020) zimemthibitisha Mbunge wa jimbo la Ruangwa mkoani Lindi, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa kuwa Waziri Mkuu kwa miaka mitano mingine (2020-2025) kwa kupata kura zote zilizopigwa na wabunge sawa na asilimia 100.

Akizungumza baada ya kuthibitishwa Mheshimiwa Majaliwa amesema amepokea uteuzi huo kwa mikono miwili na anamshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameendelea kuwapa uhai wote na kushuhudia hayo, Pia ametumia fursa hiyo kumshukuru Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa imani kubwa aliyoionesha juu yake.

"Mheshimiwa spika naomba nitumie nafasi hii kwa dhati yangu ya moyo kumshukuru sana Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupitia uwakilishi wenu. "

"Nitaendelea kushirikiana na wabunge wenzangu wote nikijua nyie ni wawakilishi wa Watanzania wanaotamani kupata maendeleo kupitia uwakilishi wenu. "

Kwa upande wake, Spika wa Bunge la 12 Mhe. Job Ndugai amesema wabunge wamemthibitisha Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, baada ya kupokea jina la Waziri Mkuu lililowasilishwa bungeni na Mpambe wa Rais na kisha wabunge kupiga kura kwa ajili ya kulithibitisha jina hilo.

"Kura zote zilizopigwa ni 350 hakuna iliyoharibika, hakuna kura ya hapana. Kura zote 350 zimemthibitisha Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, kwa hiyo ndugu wabunge Mheshimiwa Majaliwa amethibitishwa na Bunge hili kuwa Waziri Mkuu kwa kura 350 sawa na asilimia 100," alieleza Spika



**Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza na Makatibu wa Ofisi yake, Wakuu wa Idara na Vitengo pamoja na Watendaji Wakuu wa Taasisi zilizopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu baada ya kuapishwa na Rais wa Jamhuri wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli**



**Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akiwa kwenye picha ya pamoja na Makatibu wa Ofisi yake na Wakuu wa Idara na Vitengo kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu**

# SERIKALI KUIMARISHA MIFUKO YA KUWEZESHA WANANCHI KIUCHUMI

Serikali ya Awamu ya Tano, inayoongozwa na Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imejipanga kuimarisha mifuko ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ili kutoa fursa kwa wananchi kuanzisha au kuendeleza shughuli mbalimbali.

Akifungua Bunge la 12 Jijini Dodoma. Mheshimiwa Rais, Dkt. Magufuli alielezea jitihada za serikali anayoiongoza ambavyo imekuwa ikiwezesha wananchi kiuchumi kwa kuwapatia mikopo isiyo na riba ama yenye riba nafuu, ikiwemo mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na Halmashauri zetu pamoja na baadhi ya Mifuko hiyo ni Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (YDF); Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (WDF); Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wajasiriamali (NEDF); Mfuko wa Kutoa Mikopo kwa Wajasiriamali Wadogo (SELF Microfinance Fund), Mfuko wa Kudhamini Mikopo ya Mauzo ya Nje; Mfuko wa Kilimo Kwanza.

"Tutaimarisha usimamizi wa Mifuko hii na kuhakikisha Watanzania wanaifahamu,"

Sambamba na hayo Rais Magufuli alimuagiza Waziri Mkuu,kuishughulikia mifuko hiyo ili ifanye kazi kwa tija zaidi.

"Nataka Mifuko hii ikiwasaidie wananchi wa kawaida, wakiwemo machinga, akina baba na mama lishe pamoja na wajasiriamali wengine wadogo."



# MAFUNZO YA VITENDO SEHEMU ZA KAZI YAWAONGEZEA VIJANA UJUZI



Serikali kupitia Ofis ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali inatekeleza Programu ya Kukuza Ujuzi nchini ambayo inalenga kuimarisha nguvukazi iliyo katika soko la ajira kiujuzi.

Programu hiyo ya kukuza ujuzi nchini imekuwa ikitekelezwa kama hatua ya makusudi ya kukabiliana na kiwango kidogo cha ujuzi miongoni mwa nguvu kazi ya Taifa.

Moja wapo ya mafunzo yanayotolewa na kupitia programu hiyo ni Mafunzo kwa Vitendo sehemu za kazi kwa Wahitimu (Internship Training). Mafunzo hayo yanahusisha vijana waliohitimu ngazi mbalimbali za elimu ambapo wanapatiwa fursa ya kujifunza kwa vitendo katika maeneo ya kazi.

Serikali katika kuimarisha usimamizi wa mafunzo hayo iliandaa mwongozo wa kitaifa wa mafunzo ya vitendo kwa wahitimu wa vyuo (National Internship Guideline).

Toka mafunzo hayo yaanzishwe yamekuwa na manufaa kwa vijana wahitimu kutokana na kuwezeshwa kupata ujuzi wa fani mbalimbali na wengi wameweza kupata ajira na wengine kujiajiri kutokana na uzoefu walioupata katika mafunzo hayo.

“Nimeweza kujifunza mambo mengi yanayohusiana na fani yangu ya Sheria tofauti na nilivyokuwa chuoni ambapo nilijua vitu kwa nadharia tu, mafunzo haya yametuwezesha sisi vijana tuliohitimu kupata ujuzi sahihi unahitajika kwenye soko la ajira,”

***Sarah Nyoni***
***Mnufaika wa Programu ya Kukuza Ujuzi***

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# OFISI YA WAZIRI MKUU
# KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU

## SALAMU ZA PONGEZI

Menejimenti na Watumishi wa ***Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu*** wanaungana na kuwapongeza kwa dhati Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makamu wake, Mhe. Samia Suluhu Hassan na pia Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuchaguliwa na Watanzania kuongoza Serikali ya Awamu ya Tano ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Awamu ya Pili na Awamu ya Nane ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

"Tunaahidi kuendelea kushirikiana na Serikali katika kuratibu na kusimamia masuala ya Kazi, Maendeleo ya Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu ili kuchochea shughuli za kiuchumi kwa Wananchi na Taifa kwa Ujumla"

**Pia, *Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu inatoa pongezi kwa Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*.**









Simu: **+255 026 2963450/51**
Barua Pepe: **ps@kazi.go.tz**

Tovuti: **www.kazi.go.tz**

**Ofisi ya Waziri Mkuu_Kazi**




**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**Mtaa wa Kazi, Mji wa Serikali - Mtumba**
**S. L. P 2890, DODOMA**
**Barua Pepe: ps@kazi.go.tz, Simu: +255 026 2963450/51**
**Tovuti: www.kazi.go.tz**